

# UJASIRIAMALI NA UENDESHAJI WA BIASHARA KWA WASTAAFU:


Na

**BEATRICE KIMARO**

**DKT. CYRIL KOMBA**

# YALIYOMO:




- Mstaafu ni nani?
- Maana ya Ujasiriamali
- Tofauti kati ya Mjasiriamali na Mfanya biashara
- Sifa za Mjasiriamali
- Kanuni za Ujasiriamali
- Hatua za kuchukua ili uwe Mjasiriamali
- Jinsi ya Kupata Mtaji
- Makosa ambayo Mjasiriamali hapaswi Kufa

# Kustaafu ni nini?







- Ni Umri rasmi kwa mujibu wa sheria ya ajira ambapo ni miaka 60 kwa maofisa wakawaida wa serikali, miaka 65 kwa maofisa waliotajwa na katiba na huweza kuongezewa mkataba hadi miaka 75.
- Hivyo yoyote anayeacha kazi mwenyewe, kwa kujiuzulu kwa uamua, kulazimishwa, kulazimika au kwa shinikizo lolote, kuanzia miaka 45, anaitwa amestaafu!.

- Wastaafu wengi nchini huishi maisha ya dhiki baada ya kumaliza mafao waliyolipwa baada ya utumishi wa muda mrefu.

- Ni ukweli usiopingika kuwa wazee hawa huingia kwenye matumizi mabovu ya fedha pindi wanapopata malipo yao ya kustaafu kwa mkupuo.

- Fedha hizo huingizwa kwenye matumizi mabovu, uwekezaji usiokuwa na uzoefu kuleta tija iliyokusudiwa kabla ya kuishiwa na kumfanya mzee kuanza kuishi bila matumaini yoyote ya kujinasua.

- Hapa watoto huanza kutegemewa, kama wapo. Vinginevyo ndugu huhusika kusaidia kulisongesha gurudumu la maisha kwa wapendwa hawa.

***"Be Retired, But don't get Tired"***

## ,.......

- Kuna ulazima mkubwa wa kuwaandaa wazee hawa kisaikolojia kuwekeza kwa manufaa pindi watakapostaafu kujiingizia kipato cha kutosha kumudu gharama za maisha. Hili lina umuhimu mkubwa kwa sababu bado viwango vinavyotolewa havikidhi mahitaji.
- Ni wakati muafaka kwa vyama vya Ushirika Hususani SACCOS kuandaa mafunzo ya **Ujasiriamali** mara kwa mara kwa wanachama ambao wamekaribia, ambao tayari wameshataafu ili kuwaandaa kisaikolojia kukabiliana na maisha baada ya kuastaafu.


WHAT'S
YOUR PLAN
FOR
RETIREMENT?


Retirement
Planning
Happiness
Hobbies
Health care
Insurance


Why Plan
for Retirement?
Rising
healthcare
costs
Protect
post-retirement
lifestyle
Increasing
standard of living
Inflation


ENTREPRENEUR
IDEA
PLAN
GO!!!




- Neno Ujasiriamali lina asili ya Kifaransa " Entreprendre“ sawa na Kutekeleza/Kufanya shughuli fulani mwenyewe katika uwanja wa kibiashara katika maana rahisi.
- Ni sawa na kuanzisha biashara/shughuli ya kujiajiri.
- Dhana ya Ujasiriamali ina maana pana , miongoni mwa hizo ni;
  - Ni uwekezaji wa mtaji katika biashara kwa lengo la kujiajiri na kujiongezea kipato.
  - Ni ujuzi na Maarifa ya mtu katika kutumia fursa zilizopo
  - Ni uwezo Binafsi wa mtu wa kubadili mawazo na kuyaweka katika vitendo




- Ujasiriamali hauna umri. Vijana na wazee wote wanaweza kuchangamkia fursa zilizopo sokoni.
- Maandalizi na mipango mizuri inahitajika kufanikisha jambo lolote baada ya kuzikabili changamoto zitakazojitokeza.
- Ujasiriamali ni muunganiko wa maneno mawili **Ujasiri** na **mali**.

# Entrepreneur

Kwa mitazamo mbalimbali ya wasomi wana muelezea Mjasiriamali kama mtu ANAYEONGOZA, ANAYEPANGA na ALIYE NA UTAYARI juu ya hatari zozote zinazoweza kujitokeza katika biashara/shughuli yake husika.

- Mjasiriamali ni mtu ambaye ana hamasa kubwa ya kuleta mabadiliko chanya katika hali yake ya kiuchumi ambaye ana tabia za kipekee ili kufanikisha azma yake hiyo kwa kujishuhulisha (yaani kujiajiri) ili awe na hali nzuri zaidi kiuchumi
- Pia katika hali nyingine Mjasiriamali anaweza kuwa mtu yoyote ambaye anajishughulisha mwenyewe(amejiajiri) katika sekta fulani mfano: kilimo, ufugaji au biashara.



- Mchumi wa KiAustrian Joseph Schumpeter ameielezea dhana ya ujasiriamali kwa kuegemea mihimili ya UGUNDUZI na UBUNIFU, katika nyanja hizi (yaani kugundua na kubuni):-
- -Bidhaa Mpya
- -Njia Mpya za uzalishaji/uendeshaji.
- -Masoko Mapya
- -Mifumo mipya ya Vikundi na Mashirikisho.

- UTAJIRI unapatikana pindi *UGUNDUZI* unapoenda sambamba na *MAHITAJI.*
- kwa mtazamo huu tunaweza kusema ya kwamba kazi ya Mjasiriamali mstaafu ni sawa na kuunganisha mbegu za vigezo fulani katika hali ya Ugunduzi na Ubunifu ili kutengeneza ubora na thamani kwa mteja kwa imani ya kwamba thamani itakayopatikana itafidia gharama za mbegu hizo, na hatimaye kutengeneza faida ya kutosha inayompelekea kuupata UTAJIRI.






- Kwa hakika ujasiriamali ni chaguo muhimu sana kwenye karne hii ya sasa kwa wastaafu wote ili kujipatia kipato. Hivi leo kuna wastaafu wajasiriamali wengi waliofanikiwa na wengine hawajafanikiwa.
- Waliofanikiwa wanafahamu na wanaziishi sifa za wajasiriamali bora. Ni wazi kuwa huwezi kuwa mstaafu mjasiriamali bora wakati huna sifa, Ili kuwa mstaafu mjasiriamali ni lazima kuzifahamu na kuziishi sifa za mjasiriamali ambazo ni;

# SIFA ZA MJASIRIAMALI




## 1. Malengo na Mipango Dhabiti

- Malengo ni mwongozo wa kukuwezesha kufanikisha jambo lolote. Kuwa na malengo ni sifa muhimu ambayo kila mjasiriamali anapaswa kuwa nayo.
- Je, umeamua kuwa mstaafu mjasiriamali kwenye nini? Kwa ajili ya malengo yapi???
- Malengo yatakupa mipango ya kufanya ukivichanganya kwa pamoja utapata **mafanikio**.
- Umewahi kujiuliza malengo yanaweza kuwa na nguvu gani kwenye maisha yako. ***Kama ulikuwa hujui ni kwamba malengo ni kama petroli kwenye moto***

## 2. Nidhamu.





- Nidhamu ni sifa muhimu kwa mjasiriamali kwani itamtenga na mambo mengi yasiyokuwa na umuhimu. Ni lazima mstaafu mjasiriamali awe na nidhamu ya maswala kama vile matumizi ya muda pamoja na pesa.






- Kila mjasiriamali anapaswa kujinyima na kukataa vitu vyote ambavyo havimwezeshi kufikia malengo yake. Muhimu zaidi kuwa na Nidhamu Binafsi




*"Descipline is doing what you don't want to do when you don't want to do it"*

## 3. Ujasiri na Uthubutu.

- Ujasiri na uthubutu ni sifa muhimu sana kwa mjasirimali ili aweze kutekeleza malengo yake. Ujasiriamali ni swala linalohitaji ujasiri na uthubutu wa kuchukua maamuzi magumu hata kama kuna changamoto au hatari kadha wa kadha.
- Huwezi kuwekeza pesa zako kwenye mradi au biashara yoyote kama hutokuwa na ujasiri na uthubutu. Ujasiri na uthubutu hautaruhusu hofu na mashaka ya kushindwa au kupata hasara vikutawale.



# 4. Ubunifu

- Ubunifu humtofautisha mjasiriamali mmoja na mwingine. Unahitaji ubunifu ili ubuni wazo la pekee ambalo litakupa matokeo mazuri. Wajasiriamali wengi hawana ubunifu ndiyo maana wanakwama.
- Kwa mfano mjasiriamali mmoja akianzisha biashara ya kuuza kuku, basi wengine 20 wataiga. Ni lazima mjasiriamali uwe na ubunifu utakaokuwezesha kufanya mambo yenye tija.
- Ubunifu lazima uambatane nauhitaji.






## 5. Uvumilivu

- Kila jambo lina changamoto zake. Ujasiriamali una changamoto nyingi ambazo zinahitaji uvumilivu ili kuzimudu.Hivyo basi, sifa ya kuwa na uvumilivu ni muhimu sana kwa kila mstaafu mjasiriamali anayetaka kufanikiwa. Haijalishi umepata hasara au unakutana na changamoto nyingi kiasi gani, ni muhimu kuvumilia. ***"Don't Panic, Don't Force, Give Time"***

## 6. Kupenda unachokifanya

- "Fanya unachokipenda na pesa zitafuata."---Marsha SSineta
- Watu waliofanikiwa sana duniani, wanafanya kile wanachokipenda. Unapofanya kile unachokipenda ni rahisi kufanikiwa kwani utakifanya kwa **moyo**, **bidii** pamoja na **kutokata tamaa**.



## 7. Kuishi na watu vizuri

- Kila mjasiriamali anahitaji watu wengine ili kufanikisha malengo yake ya ujasiriamali. Kuishi na watu vizuri ni sifa muhimu kwa mjasiriamali kwani itamjengea soko zuri pamoja na nguvu kazi bora. Usiwadharau au kutenga watu bila sababu, Usijenge chuki au ugomvi Kumbuka kuwa watu ndio chanzo na msingi wako wa kupata faida. Watu ni Mtaji.

## 8. Mwenye kupenda kujifunza na mtafiti

- Kila mjasiriamali anatakiwa kuwa na sifa hii ili aweze kujifunza na kutafiti njia na mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kumfanya mwenye tija zaidi. Ni muhimu kukumbuka kuwa kuna wakati mjasiriamali anatakiwa kukaa chini kutafiti na kujifunza mambo mbalimbali ambayo yatamwezesha kufanikiwa kwenye kile anachokifanya.

## 9. Kujifunza kutokana na makosa

- Kama ulivyowahi kusikia mara kadhaa kuwa makosa ni shule muhimu kwa kila mtu, ndivyo ilivyo pia kwa mjasiriamali.
- Mjasiriamali anapaswa kuwa na sifa ya kupenda kujifunza kutokana na makosa ili asiyarudie tena mbeleni na wala si kuyaogopa au kuyakimbia.
- Kama uliwekeza pesa zako zikapotea, basi usiache ujasiriamali bali baini ni nini kilisababisha ukapoteza pesa zako ili ukiepuke mbeleni.
- Hudhuria semina, warsha, makongamano, maonyesho na nenda na Bidhaa zako

## 10. Bidii

- “Mafanikio huja kwa wale ambao wanafanya bidii kubwa kuyatafuta.”---Henry David Thoreau
- Bidii ni msingi wa kufanikiwa kwenye jambo au shughuli yoyote. Ni muhimu kukumbuka kuwa mjasiriamali ni mwajiri (boss) wake yeye mwenyewe. Hivyo ni muhimu kujituma na kufanya kazi kwa bidii bila kusukumwa na mtu yeyote.

# Jinsi Mstaafu anavyoweza Kujijengea tabia za Kijasiriamali




- Fanya kile kilichoko ndani ya Uwezo wako kujiendeleza na tafuta msaada pale uwezo wako unapoishia.
- Tumia Fursa zilizoko karibu nawe hata kama ni kidogo ili kuanza safari ya kijasiriamali
- Jiweke karibu na watu wenye mtazamo chanya, wenye malengo na bidii.
- Jenga uaminifu kwa kutimiza ahadi na ukikopa lipa kwa wakati.
- Jiwekee Malengo makubwa ambayo unayoweza kuyafikia. Yaandike, yaombee, yatekeleze na kuyafuatilia.
- Jenga Mtazamo chanya na Jifunze kuona mazuri katika kila hali. *Ajionavyo mtu nafsini mwake ndivyo alivyo.*
- Weka kumbukumbu za mapato na matumizi yako. *Mali bila daftari hu[potea bila habari*

# Tabia za Kukwepa ili kuwa Mjasiriamali Mstaafu Mahiri:

- UVIVU, uchukie kama ukoma
- Kupoteza muda,



Dalili za Uvivu

- Kuahirisha mambo
- Vikengeushi (Distructions)
- Visingizio. Mafanikio yako yanakutegemea wewe kwa 90%.
- Kuwa tegemezi wa mawazo wala rasilimali kwa yeyote ila wewe mwenyewe.
- Kukata tamaa.

# Nini cha Kufanya;

- Kuwa na maono
- Chagua washirika au timu sahihi
- Toa huduma au bidhaa yenye tija
- Fahamu na jali wateja
- Sikiliza maoni na ushauri wao.
- Hakikisha unakamilisha mahitaji yao.
- Tumia lugha nzuri na rafiki kwa wateja.
- Mfanye mteja aone unamthamini.
- Mfanye mteja aone kuwa umetanguliza huduma kabla ya pesa.



- Tumia pesa vyema
- Jifunze kusema hapana*“**Hapana” ni jibu dogo lakini lenye manufaa makubwa.***
- Usipuuze nafasi ya teknolojia
- Fahamu soko
- Ongeza maarifa
- Jifunze kutokana na makosa
- Jifunze kwa waliofanikiwa
- Weka vipaumbele
- Usikate tamaa



Changamoto zipo leo na kesho lakini keshokutwa hazitakuwepo tena; jambo unalotakiwa kufanya ni kutazama lengo lako na kufanya bidii kila kukikucha kuzikabili changamoto husika ili ufikie lengo lako.

“Siri ya mafanikio yetu ni kutokukata tamaa”

# Jinsi ya Kupata Mitaji:




- Akiba Binafsi
- Mikopo kutoka taasisi za kifedha hususani SACCOS (MRT wanatoa mikopo kwa wastaaafu)
- Misaada
- Kufanya Uwekezaji
- Ndugu, jamaa na Marafiki
- Kubadilisha mali na Vitu
- Mali kauli





# MAKOSA AMBAYO MJASIRIAMALI HUTAKIWI KUYAFANYA ..

- **Kujifanya unafahamu kila kitu**
- kuendesha biashara ni kujifunza na kupata uzoefu. Jitahidi kujifunza na kujijengea uzoefu kupitia maarifa mbalimbali ili uweze kuendesha biashara yako vyema kama mjasiriamali.
- **Kuanza biashara bila miundombinu**
- Ni dhahiri kuwa wengi husema "mwanzo ni mgumu" lakini ni lazima utengeneze miundombinu kadhaa. Unapoanzisha biashara kama mjasiriamali jitahidi kuweka miundombinu kadhaa ya muhimu kwanza kabla hujaanza kufanya biashara




- Kuchagua mshirika asiyefaa
- Kutazama mafanikio pekee
- Kutaka wateja wakutafute
- Kupuuza nafasi ya teknolojia
- Matumizi mabaya ya fedha
- Kupuuza maoni ya wateja
- Kuachia fursa zipite
- Kukataa ushauri wa kitaalamu
- Kutokuzingatia mahitaji ya soko
- Mbinu duni za soko



# Hitimisho:

- "Ujasiriamali siyo kazi wala cheo, wala taaluma. Bali ujasiriamali ni mchakato, ni mfumo wa maisha. Hivyo unapochagua kuwa mjasiriamali, unaufanya ujasiriamali kuwa maisha yako na hivyo huuachi kwa sababu mambo ni magumu. Badala yake unaweka imani yako kwenye mchakato mzima, ukijua ipo njia na kwa hakika njia itajitokeza mbele yako.

  "***Kwamaana Twaenenda kwa Imani sio kwa Kuona***"**.**




*Mungu Awabariki saana,*
*Nendeni Mkafanikiwe*